

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**



TAARIFA KWA UMMA

**UFAFANUZI WA TAARIFA KUHUSU MZALENDO ANAYEKWAMISHWA NA TRA NA
WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**

Mnamo tarehe 28 Novemba, 2017 iliandikwa taarifa katika mitandao ya kijamii inayoeleza mwekezaji Mzalendo mwenye kampuni ya **TRIPLE "S" Investment Co Ltd** inayozalisha maji, wine, na spirit kukwamishwa na Wizara hii kwa kutopewa stika pamoja na kuwa na vibali vyote.

Wizara ilimtafuta mwekezaji husika ili kufahamu ukweli wa jambo hili. Baada ya majadiliano alikiri kuwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji haijamkwamisha kwa jambo lolote na alipata ushirikiano mzuri pale alipohitaji huduma za wizara.

Tunapenda kuchukua fursa hii kueleza kuwa Wizara itaendelea kushirikiana na kampuni ya **Tripple S** pamoja na wawekezaji wengine kwa kuwapatia huduma na miongozo mbalimbali inayohusu Uwekezaji na Biashara.

Wizara ina dawati maalum la kusikiliza na kuzitafutia ufumbuzi kero na changamoto za wawekezaji na wafanyabiashara kupitia barua pepe **helpdesk@mit.go.tz**

Hivyo, tunapenda kuwataarifu wawekezaji wanapokutana na changamoto yoyote kuwasiliana moja kwa moja na Wizara ili kuweza kupata ufumbuzi haraka. Wizara inazidi kuwasisitiza na kuwakumbusha wawekezaji wote wa ndani na nje kufuata taratibu za kisheria ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.

Aidha Wizara inawakaribisha wawekezaji wote kuwekeza nchini Tanzania.

Imetolewa na :

*Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji
S.L.P 2996 DODOMA*

Tovuti: *www.www.mit.go.tz*

<https://www.facebook.com/mit.go.tz>